

**HOTUBA YA MHESHIMIWA CHARLES MAKONGORO NYERERE
MKUU WA MKOA WA RUKWA WAKATI WA MAKABIDHIANO YA
OFISI TAREHE 23 JUNI, 2023**

- **Mhe. Queen C. Sendiga, Mkuu wa Mkoa wa Manyara,**
- **Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (MNEC),**
- **Ndugu Gerald M. Kusaya, Katibu Tawala Mkoa wa Rukwa,**
- **Katibu wa CCM Mkoa,**
- **Wakuu wa Seksheni na Vitengo Sekretarieti ya Mkoa,**
- **Wakuu wa Taasisi za Umma na Binafsi,**
- **Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya,**
- **Makatibu Tawala Wilaya,**
- **Mstahiki Meya wa Manispaa ya Sumbawanga,**
- **Wahe. Wenyeviti wa Halmashauri,**
- **Viongozi wa Dini,**
- **Machifu,**
- **Viongozi wa Vyama vya Siasa,**
- **Waandishi wa Habari,**
- **Wageni waalikwa,**
- **Mabibi na Mabwana.**

Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.....

Awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha sisi sote kukutana mahali hapa tukiwa wazima na wenye afya njema. Kipekee nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini katika nafasi hii na kunihamishia katika Mkoa huu wa Rukwa. Ninamshukuru sana.

Ndugu Washiriki, tumekutana hapa kwa ajili ya tukio la makabidhiano kati yangu na Mhe. Queen Cuthbert Sendiga Mkuu wa Mkoa aliyehamishiwa Mkoa wa Manyara akitokea Mkoa wa Rukwa. Tukio hili ni la kipekee kwasababu linahusisha Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa wawili ambao wamebadilishana vituo vyao vya kazi.

Ndugu Washiriki, Rai yangu kwa Watumishi wa Umma ni kuendelea kufanya kazi kwa bidii, uaminifu na uzalendo ili kuendelea kuwatumikia Wananchi wa Rukwa. Aidha, mnatatua kero mbalimbali za Wananchi na Watumishi wa ngazi zote kwa wakati.

Ndugu Washiriki, ujumbe wangu kwa wananchi wa Mkoa wa Rukwa ni kuendelea kuwatumikia kwa nguvu zote ili kwa kushirikiana na wao wenyewe tuweze kuleta maendeleo ya Mkoa wetu wa Rukwa. Nawaomba sana Wanarukwa wanipatie ushirikiano katika kutekeleza majukumu yangu ya kila siku.

Ndugu Washiriki, Watumishi wote wa Umma mnao wajibu wa kuhakikisha kuwa mnafanya kazi kwa ushirikiano (Team Work) ili tuweze kufanya kazi yenye matokeo. Upo msemu usemao “Umoja ni Nguvu na Utengano ni Udhaifu”. Tukifanya kazi zetu kwa kushirikiana tutatimiza malengo ya kuwaletea maendeleo wana Rukwa.

Ndugu Washiriki, leo ni tukio la makabidhiano ya Ofisi tu, yapo mambo mengi ambayo nitaendelea kuzungumza na makundi mbalimbali ya wananchi kwa muda utakaopangwa.

Mwisho, Niwashukuru sana wote mliokusanyika katika tukio hili. Niseme tu kuwa sina cha kuwalipa zaidi ya kuwarudishia upendo kwa kuwatumikia kwa moyo.

Mungu Ibariki Tanzania!!!

Mungu Bariki Mkoa wetu wa Rukwa!!!

Asanteni sana kwa kunisikiliza.

Charles Makongoro Nyerere

MKUU WA MKOA WA RUKWA